Jarida La MELI

TOLEO LA 6 JANUARI - MACHI 2023

USEMI WA KAZI IENDELEE WADHIHIRIKA.. UK. 2

Ushirikiano wa CCTTFA na MSCL.. UK. 4

WFP wafurahishwa na maendeleo ya miundombinu ya usafiri... UK. 9

Muonekano wa Meli ya MV Mwanza Hapa Kazi Tu wakati ikishushwa kutoka kwenye chelezo kwenda kwenye maji ziwa Victoria tarehe 12 Februari, 2023 bandari ya Mwanza kusini.

MV MWANZA YASHUSHWA ZIWANI KWA MAFANIKIO

Na. Abdulrahman Salim

Baada ya wananchi kusubiri kwa hamu tukio la kushushwa kwa meli ya MV Mwanza Hapa Kazi Tu kutoka kwenye chelezo na kuingia kwenye Ziwa Victoria hatimaye tarehe 12.2.2023 subira hiyo ilifikia tamati baada ya meli hiyo ya kwanza kwa ukubwa katika ukanda wa Nchi za Maziwa Makuu barani Afrika kugusa maji katika zoezi ambalo lilifanikiwa kwa asilimia 100.

Akizungumza wakati wa hafla kwa niaba ya Waziri wa Wizara Profesa Makame Mbarawa, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Atupele Mwakibete ameishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo ya kimkakati iliyopo katika Mkoa wa Mwanza na kuongeza kuwa Serikali itaendelea kuwekeza fedha kwa miradi inayotekelezwa na Wizara hiyo kupitia Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL).

"Serikali iliamua kujenga meli kubwa ili kukidhi mahitaji ya soko ambayo yanatarajiwa kuongezeka hasa pale mradi mkubwa wa ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza utakapokamilika. Aidha, kujengwa kwa meli hii kutasaidia kufungua masoko mapya ndani na nje ya nchi kwa kuanzisha safari mpya zitakazosaidia kurahisisha shughuli za kibiashara, kikazi, utalii na safari binafsi kwenye maeneo mengi zaidi ya ilivyo sasa."

"Mbali na mradi huu wa MV Mwanza wenye gharama ya Shilingi Bilioni 109.15, Mheshimiwa Rais ametuelekeza Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwenye Bajeti ya Mwaka wa fedha wa 2022/2023 kwenye Ziwa Tanganyika tutengeneza meli mpya mbili, moja ni ya abiria na mizigo na nyingine ni ya mizigo pekee, kwa niaba ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi nitumie fursa hii kumshukuru sana Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutupatia fedha

Inaendelea Ukurasa wa 2..

USEMI WA KAZI IENDELEE WADHIHIRIKA KWA MV MWANZA

Na. Jannath Ali

Usemi wa "Kazi Iendelee" umejipambanua kiutendaji mbele ya macho ya watanzania waliohudhuria hafla ya ushushwaji wa meli ya MV Mwanza Hapa Kazi Tu kutoka kwenye chelezo kuingia katika Ziwa Victoria, hiyo ikiwa ni hatua ya pili muhimu kati ya hatua nne za maisha ya meli.

Usemi huo umebainishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) Ndg. Eric Hamissi wakati akitoa taarifa fupi ya mradi huo mbele ya mgeni rasmi Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) Mhe. Atupele Mwakibete katika hafla hiyo iliyofanyika bandari ya Mwanza Kusini.

"Mradi huu ulipokelewa kutoka awamu ya tano ukiwa umefikia asilimia 45, lakini mpaka kufikia kushushwa kwa meli hiyo ujenzi umefikia asilimia 82, huku mkandarasi wa mradi huo Gas Entec Ship- Building Engineering kwa kushirikiana na Kang Nam Corporation ya nchini Korea Kusini, ameshalipwa asilimia 88 ya pesa ambayo ni sawa na bilion 93.8, na hadi kukamilika kwake mradi huu utagharimu kiasi cha shilingi bilioni 109.95 za kitanzania " alieleza Ndg. Eric

Alisema kuwa meli hiyo inatarajiwa kuwa na jumla ya madaraja sita ambayo ni VVIP; daraja maalumu kwa viongozi wa kitaifa wawili, Daraja la VIP litakalobeba watu mashuhuri wanne katika chumba kimoja, daraja la kwanza litakalobeba jumla ya watu 60, daraja la biashara litakalobeba watu 100, daraja la pili litakalobeba watu 200 na daraja la uchumi litakalobeba abiria 834 hivyo kufanya jumla ya abiria 1,200.

Katika hotuba yake mgeni rasmi wa hafla hiyo Mhe. Mwakibete aliielekeza Bodi wa Wakurugenzi ya MSCL kuisimamia vyema Menejimenti ya MSCL ili kuhakikisha miradi yote inatekelezwa na Serikali kama ilivyopangwa na kuleta thamani ya fedha iliyowekezwa ikiwa ni pamoja na kuendelea kuusimamia mradi wa MV Mwanza Hapa Kazi tu ili kuhakikisha unakamilika ndani ya muda uliopangwa na meli kuanza kuwahudumia wananchi.

"Nitoe rai kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) kuhakikisha inajipanga kuendelea kuboresha bandari katika Ziwa Victoria ili meli hii iweze kutia nanga bila ya shida wakati itakapoanza safari zake."

Mhe. Mwakibete aliongeza kuwa ukamilifu wa meli ya MV Mwanza utasaidia kuanzishwa kwa masoko mapya Afrika Mashariki, kupanuka kwa shughuli za kibiashara, kikazi pamoja na Utalii kwani meli hiyo itakuwa ya kisasa zaidi na yenye mwendo wa kasi kuliko meli zilizopo sasa inayokadiliwa kubeba abiria wengi na mizigo mingi.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na viongozi mablimbali wa serikali wakiwemo, wakuu wa mikoa ya kanda ya ziwa, mawaziri, wabunge, wakuu wa taasisi mbalimbali za kiserikali na zisizo za kiserikali, wafanyabiashara na wananchi kutoka mikoa mbalimbali.

Meli ya MV Mwanza Hapa kazi Tu ujenzi wake ulianza mapema mwezi Januari mwaka 2019 na unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti mwaka 2023 na kuanza safari zake katika Ziwa Victoria.

MV MWANZA YASHUSHWA KWENYE ZIWA ....

InatokaUkurasa wa 1..

za miradi hii yote," alisisitiza.

Sanjari na hayo, Mhe. Mwakibete ameielekeza Menejimenti ya MSCL kubainisha vijana waliopata utaalamu kupitia mradi huo waweze kutumika kadri ya mahitaji ya kampuni yatakavyojitokeza ili nguvu kazi yenye uzoefu isipotee.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa MSCL Ndg. Eric Hamissi ameeleza kuwa meli hiyo ina uwezo wa kubeba abiria 1200, tani 400 za mizigo, magari madogo 20 na magari makubwa matatu; Na itakapokamilika itahudumia bandari zote kuu za Ziwa Victoria ikiwemo bandari ya Kemondo, Bukoba, Mwanza, Musoma; bandari ya Portbell na Jinja za nchini Uganda pamoja na bandari ya Kisumu nchini Kenya.

Ameeleza kuwa meli hiyo itakuwa na madaraja sita ambayo ni VVIP itakayokuwa maalum kwa viongozi wa kitaifa, Daraja la VIP ambalo litabeba watu mashuhuri, Daraja la Kwanza, Daraja la Biashara, Daraja la Pili na Daraja la Uchumi.

"Ndani ya meli hii pia kutakuwa na burudani; kutakuwa na sehemu ya 'Lift' hasa kwa watu wenye changamoto ya kupanda ngazi, Hali ya Ulemavu au wagonjwa; sehemu ya Zahanati na sehemu ya wamama wajawazito. Tunatarajia meli hii itakuwa inatumia masaa 10 pekee kwenda bandari ya Portbell nchini Uganda lakini pia itaenda Musoma mkoani Mara," ameelezea Ndg. Eric Hamissi.

Meli hiyo inayojengwa na Mkandarasi GAS Entec kwa ushirikiano na Kagnam Corporation za nchini Korea pamoja na Suma JKT ya Tanzania itagharimu Shilingia Bilioni 109.15 hadi kukamilika kwake.

BODI MPYA MSCL YAPONGEZA MAENDELEO YA MIRADI BANDARINI

Na. Doreen Mussa

Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) imepongeza hatua iliyofikiwa ya utekelezaji wa miradi inayoendelea kutekelezwa na Kampuni hiyo katika eneo la bandari ya Mwanza Kusini, Jijini Mwanza.

Pongezi hizo zilitolewa na wajumbe wa Bodi hiyo muda mfupi baada ya uzinduzi wa Bodi hiyo na kupata fursa ya kutembelea na kukagua miradi ya ujenzi wa Meli mpya ya MV Mwanza na Ukarabati wa meli ya mizigo ya MV Umoja tarehe 14.1.2023.

Wakati akitoa pongezi zake kwa niaba ya Wajumbe, Mwenyekiti wa Bodi hiyo Mej. Jen. Mst. John Mbungo alitoa pongezi kwa menejimenti ya MSCL katika uangalizi wa utekelezaji wa miradi hiyo na kuwasisitiza kuwa makini na uwekezaji ambao Serikali imeufanya na hivyo kuwataka kuwa na mipango thabiti itakayoleta tija kwa Serikali.

"Kutokuwepo kwa bodi kumeathiri sana maendeleo ya Kampuni na maendeleo ya Kampuni yanategemea sana maamuzi ya vikao vya Bodi, hivyo naamini tupo kwa ajili ya kuisimamia Kampuni na tutahakikisha tunafanya hivyo kwa maendeleo ya Kampuni na Nchi kwa jumla," Alisisitiza.

Kwa upande wake Mjumbe wa Bodi hiyo Bi. Stella alifurahishwa na namna ambavyo meli ya MV Mwanza ilivyojengwa kisasa kwa kuzingatia utunzaji wa mazingira kwa usalama wa viumbe vwanaoishi kwenye maji pamoja na abiria wake.

"Leo baada ya kutembelea hii meli mpya ambayo inajengwa hapa ya MV Mwanza nimeona kama hiyo ndoto inakwenda kutimia kutokana na maelezo ya wakandarasi ambao wanahusika na ujenzi wa meli hii, tunaona maeneo mengi ya kiusalama yamezingatiwa sio tu usalama wa abiria lakini pia pale ambapo kunahitajika kutenganisha mafuta na maji na zile taka zinazozalishwa melini kuna sehemu ya kuhifadhiwa ili meli itakapofika bandarini ziweze kupelekwa katika maeneo ambayo zinaweza kuchakatwa" Alisema.

Bodi ya Wakurugenzi ya MSCL inaundwa na wajumbe 9 na Mwenyekiti Mej. Jen. Mst. John Mbungo akikamilisha idadi ya kuwa 10 ambapo baada ya ziara hiyo wanatarajiwa kupatiwa mafunzo

Mrakibu wa Meli wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) Mha. Abel Gwanafyo (kulia) akitoa maelezo ya maendeleo ya Miradi ya Ujenzi wa Meli mpya ya MV Mwanza Hapa Kazi Tu pamoja na Meli ya mizigo ya MV Umoja (Haipo pichani) kwa Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya MSCL katika bandari ya Mwanza Kusini.

Ushirikiano wa CCTTFA na MSCL kuunganisha fursa za kibiashara na nchi jirani

Na. Shani Chogero

Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) imetia saini makubaliano ya ushirikiano (MoU) na Wakala wa Uwezeshaji wa Usafiri wa Ushoroba wa kati (CCTTFA) katika kuimarisha utafutaji wa masoko katika nchi zinazopakana na Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria ikiwa ni sehemu ya maandalizi kwa meli zinazoendelea kujengwa na Serikali chini ya MSCL.

Akizungumza baada ya kutia saini makubaliano hayo Mkurugenzi Mtendaji wa MSCL Ndg. Eric Hamissi alisisitiza kuwa kwa miaka kadhaa CCTTFA wamekuwa wadau wakubwa wa kuchagiza maboresho ya huduma za usafiri na usafirishaji kwa njia ya maji na hivyo kuwashukuru kwa kuendelea kutoa ushirikiano katika kufanya utafiti wa fursa zinazopatikana nchi za jirani

"Makubaliano haya ni muendelezo wa mkataba uliosainiwa miezi kadhaa nyuma ikiwa na lengo la kuimarisha miundombinu ya utendaji kazi katika taasisi zetu hizi na hii leo kusaini matumizi ya fedha hizi ambazo zitapelekea kufahamu fursa za kimasoko zinazopatikana nchi jirani ni hatua nzuri, kwani itasaidia pia kuzitangaza fursa hizo kwa wafanyabiashara na wakulima waliopo nchini kwetu kupitia majukwaa yetu ya habari."

Aidha, Ndg. Eric aliongeza kuwa mkataba huo utadumu kwa miaka mitatu na kuwa muda huo unaweza kuongezeka kulingana na mahitaji ya kuboresha huduma katika ukanda wa nchi za maziwa makuu hasa kwa Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria ambayo yapo katika mipaka ya CCTTFA.

"Potential routes (Safari tarajiwa) ziko nyingi sana, tumeshafikiria kwenda Jinja (Uganda) na meli mpya hii (MV Mwanza) na hata MV Umoja itakapoanza, tumefikiria kwenda Kisumu (Kenya), kwa Ziwa Victoria, lakini kwa Ziwa Tanganyika tuna route (safari) ya kwenda Mpulungu Zambia, lakini nani alitunyima kwenda DRC, Kalemie, nani alitunyima kwenda Bujumbura, Burundi au Uvira, hakuna aliyetunyima na utafiti wa masoko unakuja kutoa majibu ya Je, kuna Facilities (miundombinu) kule kwa meli yetu kutoa huduma?" Alifafanua.

Makubaliano hayo ya awamu ya pili yamefanya zaidi ya shilingi milioni 375 kusainiwa katika hafla fupi iliyohudhuriwa na wakuu wa taasisi hizo pamoja na menejimenti zao tukio lililofanyika katika ukumbi mdogo wa mikutano uliopo makao makuu ya MSCL, Jijini Mwanza.

Akizungumza kwenye hafla hiyo Katibu Mtendaji wa CCTTFA, wakili Okandju Okonge Flory, aliahidi kuendeleza ushirikiano baina ya taasisi hizi kwa lengo la kuboresha huduma za usafirishaji kwenye Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika.

"Katika kutekeleza mpango mkakati wa taasisi yetu tuna wajibu wa kuchochea na kuendeleza usafirishaji wa kwa njia ya maji kupitia maziwa yanayopakana nchi wanachama wa Ushoroba wa Kati ambayo ni Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika na kampuni ya huduma za meli ni mdau mkubwa kwenye kutimiza azma hiyo na tunaahidi tutaendeleza ushirikiano wetu kwani mafanikio yenu ni faida kubwa kwa wananchi wetu wa ukanda huu" alisema Wakili Okandju.

Makubaliano hayo ni muendelezo wa makubaliano ya awali baina ya taasisi hizi mbili ambayo yalisainiwa mwezi septemba 2020 kwa ajili ya ufadhili wa kusomesha watumishi wa MSCL ili kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao.

CCTTFA ni taasisi ya kikanda inayoundwa na nchi tano ambazo Tanzania, Uganda, Rwanda, Burundi na DRC ambazo makao makuu yake ni jijini Dar es Salaam

Mkurugezi Mtendaji wa MSCL Ndg. Eric Hamiss (kushoto) pamoja na Katibu Mtendaji wa CCTTFA Wakili Okandju Okonge Flory, wakitia saini Mkataba wa Makubaliano ya Ushirikiano (MOU) katika ofisi za Makao Makuu ya Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) jijini Mwanza.

HABARI PICHA

Abiria mbalimbali wakiwa katika Mwalo wa Kirumba wakiisubiri Meli ya MV Clarias inayofanya safari zake kutoka Mwanza Kwenda Visiwa vya Gana na Godziba na kurudi.

Wanafunzi wa kidato cha nne wa Shule ya Sekondari Kilimani ya jijini Mwanza wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kumaliza ziara yao ya kimafunzo ya kutembelea mradi ujenzi wa meli mpya ya MV.Mwanza



Baadhi ya wanawake watumishi wa MSCL wakiwa katika maadhimisho ya siku ya wanawake Duniani iliyofanyika kimkoa wilaya ya kwimba mkoani Mwanza tarehe 8 Machi 2023.

Mkuu wa kitengo cha Masoko na Uhusiano kwa Umma Ndg. Anslem Namala akimwelekeza Naibu Waziri , Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi,Sekta ya Uchukuzi (wa katikati) Mhe Atupele Mwakibete (mb) wakati wa uzinduzi wa kushusha meli ya MV Mwanza iliyofanyika February 2023.



KATUNI

Na. D. Mligwa

Watumishi wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kumaliza mafunzo ya namna ya kusimamia shughuli za operesheni za meli katika bandari ya Dar-es-salaam.

TUFUATE KWENYE MITANDAO YETU YA KIJAMII

mscltz **Meli Yetu TV**

Baadhi ya wajumbe wa Bodi ya wakurugenzi wa MSCL wakiwa katika picha ya pamoja na mabaharia wa New Victoria" Hapa Kazi Tu"

BODI MPYA YA MSCL YAKUMBUSHWA MAJUKUMU YAKE

Naibu Waziri Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Atupele Mwakibete ameitaka Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya Humuda za Meli (MSCL) kusimamia vyema matumizi ya fedha zilizowekezwa na Serikali kwenye miradi inayotekelezwa na Kampuni hiyo ili kuteta tija katika maboresho ya usafiri kwa njia ya maji.

Akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi wa bodi hiyo Mhe. Mwakibete alisema kuwa Serikali imewekeza fedha nyingi katika miradi ya ujenzi na ukarabati wa meli katika Ziwa Victoria, Tanganyika na Ziwa Nyasa na hivyo ni jukumu la Bodi hiyo kuona fedha za Serikali hazipotei.

"Serikali imetenga fedha zaidi ya bilioni 100 na fedha hizo zimehusisha ujenzi na ukarabati wa meli hivyo bodi mjipange kusimamia fedha hizo ili tuone matokeo ya uwekezaji wake", alisema Mhe. Mwakibete.

Aidha ameiahidi menejimenti ya MSCL kua Serikali itaendelea kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili kampuni hiyo ikiwemo kuendelea kulipa mishahara mpaka pale MSCL itakapoweza kujiendesha kwa faida.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya MSCL Mej.Jen. Mst. John Mbungo alitumia fursa hiyo kuhihakikishia Serikali kwamba bodi hiyo itajitahidi kutekeleza majukumu waliyokabidhiwa kwa weledi wa hali ya juu ili uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali uweze kuleta tija.

"Nitumie fursa hii Kumshukuru Rais wa Awamu ya Sita Dkt. Samia Suluhu Hassana kwa kuniteua na kunipa jukumu hili ambalo naendelea kuahidi kulitekeleza kwa ufanisi kwa ushirikiano na wajumbe ambao kwa kweli pia nimshukuru Mhe. Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Profesa Mbarawa kwa kuteua wajumbe wenye weledi katika sekta hii ili tuweze kushauriana na kutimiza azma ya serikali kwenye sekta hii."

Kwa upande wake kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MSCL Mha: Abel Gwanafyo alimuhakikishia Mhe. Mwakibete kua watendaji wote wa MSCL wataendelea kuchapa kazi kwa bidii kwa kushirikiana na bodi mpya uku ikisimamia misingi ya kazi na kupiga vita vitendo vyote vya uzembe na ubadhirifu wa mali za Umma ili kuwezesha uwekezaji unaofanywa na Serikali kwenye taasisi hii kuleta tija.

Aidha alimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa kutenga muda wake kuja kuzindua bodi kwani kuzinduliwa kwa bodi hii kunazidi kuleta hamasa ya utendaji kwa menejimenti na watumishi wote

Bodi mpya ya wakurungenzi ya MSCL iliyozinduliwa ina jumla ya wajumbe 10 na tayari imeshaanza kutekeleza majukumu yake

SHIPCO WAPATA SOMO ...

Inatoka Ukurasa wa 10..

Utawala kutoka SHIPCO Bi Saada Ali alisema "ziara ilikua nzuri tumefarijika sana, tumejifunza mambo mengi, tunaahidi kuyafanyia kazi na kuboresha pamoja na kuendeleza mashirikiano baina ya mashirika yetu mawili."

Zira hiyo ya siku tatu imefanyika kutekeleza maelekezo ya Serikali ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano ya Tanzania.

‘Sio Chief ni Mama’

Mha. Esther Josbell Sikazwe

Na. Doreen Mussa Mligwa

Kila tarehe 8 Machi ya kila mwaka ni Siku ya Wanawake Duniani ambapo wanawake hupatiwa heshima kutokana na ushiriki wao kwenye sekta mbalimbali.

Lakini pia ninahusika na usimamizi wa mafuta ya meli kwa kuhakikisha meli imekunywa mafuta kwa wakati na kwa kiwango kinachotakiwa yametumika kama yalivyopaswa kutumika.

ana na suala hili lakini baadae alinielewa na kunipa ushirikiano. Linapokuja suala la familia kwangu mimi sio chief engineer (mhandisi mkuu) mimi ni mama natimiza

Katika kuazimisha siku hiyo wanawakewa sekta mbalimbali walishiriki kikamilifu maonesho hayo yaliyofanyika kimkoa Wilayani Kwimba, Mkoani Mwanza.

Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) imebarikiwa kuwa na wanawake wanaofanya kazi katika vitengo mbalimbali; Makarani, Mabaharia, Maafisa Utumishi, Uhusiano, Mawasiliano, Masoko, Wanasheria, Wahasibu na Wahandisi katika kuhakikisha shughuli za Kampuni zinaleta tija kwa maendeleo ya Taifa.

Mhandisi Esther J. Sikazwe ni Mhandisi mkuu wa meli ya New Butiama Hapa Kazi Tu ambaye anawakilisha kundi la wanawake wa MSCL ambao wana mchango mkubwa katika kuhakikisha Kampuni inaleta tija kwa wananchi kwa kitengo chake kinatimiza majukumu yake kwa ufanisi.

Jarida la Meli lilipata fursa ya kuongea naye machache ambayo yanaakisi safari yake kama mhandisi mwanamke katika kuadhimisha siku hii muhimu kwa wanawake wote duniani, safari ambayo ilianzia mkoani Iringa. Mazungumzo hayo yalianza hivi.

Swali: Ni yapi majukumu yako kwenye meli ya New Butiama Hapa Kazi tu?

Jibu: Nafanya kazi kama mhandisi mitambo ambapo jukumu langu kubwa ni kuhakikisha shughuli zote zinazohusu mitambo ya meli kwa sehemu ya juu pamoja na huku kwenye mtambo mkuu maarufu kama ‘engine room’ zinafanya kazi pamoja na pia kuangalia usalama wa mitambo kwa jumla.

Swali: Je, ni changamoto gani unazokumbana nazo katika kutimiza majukumu yako?

Jibu: (alitabasamu na kuendelea) Changamoto ni nyingi kwa kweli, lakini kubwa ni kutokuaminiwa yaani mtu akiona ni mwanamke anakosa uaminifu linapokuja suala la mitambo, lakini namshukuru Mungu nina imani na kuwa ninaweza na ninastahili kuwepo hapa kingine ni bidii katika kazi inanifanya nisione changamoto kama kikazwo lakini naziona kama chachu ya kuendelea mbele.

Swali: Una uzoefu wa miaka mingapi katika kazi hii? Na ni mwaka upi ulikuwa mgumu kwako katika utendaji wa kazi?

Jibu: Fani ya ufundi nina zaidi ya miaka 10 lakini hapa kwenye Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) sina muda mrefu sana nimejiunga 2019 au 2020. Lakini katika miaka hiyo kiukweli mwaka wangu wa kwanza ulikua mgumu sana kwa sababu nilikua ndo nimetoka chuo na nilikabidhiwa kujiunga na timu ilikua inahusika na matengenezo ya meli ya MV Victoria meli ambayo niliwahi kuifanyia mafunzo kwa vitendo. Kiukweli nilipata tabu kuzoea mazingira, kulikua na hali ya kutoaminika kwa sababu mimi ni mwanamke lakini nashukuru msimamizi mkuu wa mradi Mhandisi Abel Gwanafyo alinipa moyo na ushirikiano mkubwa ambao ulinifanya niweze kuzoea mazingira.

Swali: Familia yako na jamii unayoishi nayo nje ya mazingira ya kazi inakuchukuliaje kutokana na kazi unayofanya?

Jibu: Kiukweli, mume wangu, watoto na wazazi ni waelewa na wanatoa ushirirkiano wa kutosha, japo baba yangu mzazi alionesha kutokukubali-

majukumu yangu bila kujali cheo changu ,kwa upande wa jamii uelewa bado ni mdogo hawaelewi kwamba mwanamke anaweza kufanya kazi yoyote ile aitakayo, situmii nguvu kuwaelewesha japo naamini wataelewa tu taratibu wataelewa

Swali: Ni upi wito wako kwa wanawake wengine wanaotamani kujiunga kwenye fani ya uhandisi

Jibu: Cha kwanza kutia nia, kujiamini, kusoma kwa bidii hasahasa masomo ya sayansi kuanzia sekondari na kutembea katika ndoto zao bila kukatishwa tamaa na kitu chochote. Na wazazi wasiwakatishe tamaa kwani mwanamke anaweza kuwa chochote hata ikitokea wakitaka kuwa wahandisi, nitawasimamia japokuwa kwa bahati mbaya hakuna anayetaka kuwa muhandisi, wao wanataka kuwa madaktari itanibidi niwasimamie huko wanakotaka hakuna namna.

Swali: Ni upi mpango au malengo yako ya baadae?

Jibu: Kwa baadae nitahitaji kujiendeleza kimasomo lakini sitotaka kutoka nje ya fani ya uhandisi maana naamini elimu haina mwisho kuna vingi vya kujifunza kwenye uhandisi.

Mhandisi Esther Sikazwe ameolewa na ana watoto wawili; wote wa kike. Anaishi na familia yake jijini Mwanza huku akiendelea na majukumu yake kama mhandisi kwenye meli ya New Butiama Hapa Kazi tu. Kawaida hutoka nyumbani saa moja asubuhi na kurudi majira ya saa kumi na mbili jioni na akiwa nyumbani hufanya shughuli zote akiwa kama mama.

WFP wafurahishwa na maendeleo ya miundombinu ya usafiri

Na Shani Chogero

Mwakilishi wa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) nchini Tanzania Bi. Sarah Gibson amefurahishwa na maendeleo ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Serikali chini ya Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) jijini Mwanza.

"Nimefurahi kua hapa kuona hatua kubwa ya maendeleo ya miradi ya MV Mwanza na MV Umoja na namna ambavyo taasisi za Serikali ya Tanzania pamoja na nchi Jirani ya Uganda zinavyoshirikiana, ni wakati sasa umefikia wa kuimarisha zaidi ushirikiano wetu na naamini nitarudi tena baada ya miradi kukamilika na hata kushiriki katika uzinduzi wa miradi hii,

Katika Ziara hiyo ya Siku moja Bi. Sarah alipata fursa kutembelea mradi wa ujenzi wa meli mpya ya MV Mwanza pamoja na ukarabati wa meli ya mizigo ya MV Umoja pamoja na kupata taarifa za kina juu ya mipango ya Serikali katika kuimarisha usafiri kwa njia ya maji katika ujenzi wa meli mpya, uboreshaji wa miundombinu ya bandari pamoja na ukarabati wa meli zilizopo zilizokuwa zikitoa huduma katika Ziwa Victoria.

Akizungumza wakati wa kutembelea miradi hiyo Bi.Sarah alisema "Nimefurahi kua hapa kuona hatua kubwa ya maendeleo ya miradi ya MV Mwanza na MV Umoja na namna ambavyo taasisi za Serikali ya Tanzania pamoja na nchi Jirani ya Uganda zinavyoshirikiana, ni wakati sasa umefikia kuona jinsi ambavyo tutaweza kuimarisha zaidi ushirikiano wetu wakati miradi hiyo inapoendelea kukamilika na naamini nitarudi tena baada ya miradi kukamilika n ahata kushiriki katika uzinduzi wa miradi hii,"

WFP ni miongoni mwa wadau wa kimkakati katika usafirishaji wa shehena za vyakula kupitia ushoroba wa kati kwa ushirikiano ulioanzishwa mwaka 2018. Ushirikiano huu unaunganisha sekta mbalimbali zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ikiwemo TPA, TRC, MSCL pamoja na sekta binafsi.

Aidha Meneja Masoko na Uhusiano kwa umma wa MSCL ndugu Anselm Namala alisema, WFP wamepata faraja kuona MSCL na Serikali kwa ujumla iko makini katika kutekeleza miradi ambayo inakwenda kua sehemu ya mnyororo wa usafirishaji wa mizigo kutoka bandari ya Dar es salaam hadi bandari ya Mwanza na Kwenda moja kwa moja nchini Uganda na hatimaye Sudan ya Kusini.

"Moja ya ajenda yao kubwa sana ilikuwa ni kuangalia wapi umefikia mradi wa MV Umoja kwa hakika wamefurahi kuona mradi huu unakwenda vizuri na zaidi kupata maelezo ya kuwahakikishia ya kwamba mradi huu utakamilika mapema mwaka 2023 na vile vile wakaona kuwa kuna fursa ya meli hii kubwa ya MV Mwanza kwamba sit u inasafirisha abiria lakini pia inasafirisha shehena za mizigo."

WFP na MSCL wanataendeleza ushirikiano wao wa kufanya kazi pamoja kipindi tu miradi mipya itakapokamilika hivi karibuni.

Bi Saraha Mwakililishi wa shirika la Mpango wa chakula duniani (WFP) akiwa katika picha ya pamoja Wadau wa sekta ya usafirishaji kutoka MSCL na TRC alipotembeled mradi wa ujenzi wa MV.Mwanza na ukarabati wa meli ya MV. Umoja bandari ya Mwanza kusini.

Wanafunzi wa Shule ya Sekondari wapata somo MV Mwanza

Na Doreen Musa

Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Anjelina Mabula wameishukuru Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) kwa kuwapa fursa ya kujifunza kwa vitendo masomo wanayosoma darasani kupitia mradi wa ujenzi wa meli mpya ya MV Mwanza.

Wakiongea katika nyakati tofauti wanafunzi hao wa kidato cha pili na cha kwanza wameahidi kuwa mabalozi wa usafiri kwa njia ya maji kupitia elimu waliyoipata baada ya kutembelea meli kadhaa za MSCL zilizopo katika bandari ya Mwanza Kusini.

Mwananfunzi wa Kidato cha Pili Irene Kaman alikiri kuona faida ya kujifunza somo la Jiografia na Fizikia kwa kuona kwa vitendo namna masomo hayo yanavyotumika katika fani ya uongozaji wa meli.

"Nimefurahi kuona baadhi ya vitu ambavyo tumejifunza kwenye Jiografia na Fizikia, nawashukuru wazazi kwa kuniruhusu kuja kwenye ziara hii."

Naye mwanafunzi Jackline Johnbosco alisema "Nashukuru kwa ziara hii nimejifunza vingi, kikubwa ni cherezo ambayo siifahamu, nitakuwa balozi kwa wanafunzi wenzangu kuhusu meli zilizopo."

Emanuel Isaya ni mwalimu wa shule hiyo ambaye kwa upande wake aliushukuru uongozi mzima wa MSCL kwa kuwapokea wanafunzi hao na kuwapa ushirikiano na kuahidi kuwashawishi waalimu wengine na shule nyingine kuitembelea miradi hiyo na kujifunza kwa vitendo.

Wakati akitoa taarifa ya meli ya MV Mwanza Kaimu Meneja Mradi Mhandisi Elias Kivara alisema kuwa mradi huo umefikia asilimia 82 na meli hiyo ina uwezo wa kubeba abiria 1,200 tani 400 za mizigo, magari madogo 20 na makubwa matatu.

"Meli hii ina urefu wa mita 92.6 na upana wa mita 17 na inatumia lita 35,000 na itakuwa na uwezo wa kutembea kwa masaa 6 hadi 7 kutoka Mwanza hadi Bukoba, Mkoani Kagera, gharama za mradi ni shilingi Bilioni 109," alisema.

Wanafunzi hao pia walipata fursa ya kutembelea Chelezo, meli ya MT Ukerewe, Meli ya MV Clarias na mradi wa ukarabati wa meli ya mizigo ya MV Umoja.

SHIPCO WAPATA SOMO KUTOKA MSCL

Na Shani Chogero

Wakurungezi Shirika la Meli Zanzibar (SHIPCO) wameipongeza Serikali ya Muungano wa Tanzania kwa uwekezaji wa miradi mbalimbali inayotekelezwa na Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) katika kuimarisha usafiri wa njia ya maji katika maziwa makuu.

Pongezi hizo zimetolewa baada ya timu ya wakurugenzi hao kutembelea miradi ya Ujenzi wa meli mpya ya MV Mwanza, ukarabati wa meli ya mizigo ya MV Umoja pamoja na miradi iliyokamilika ya New Victoria Hapa Kazi Tu pamoja na New Butiama Hapa Kazi Tu zinazotoa huduma katika Ziwa Victoria.

Mkurugenzi wa Masoko Utafiti na Mipango SHIPCO Ndg. Jabir Sheha Amour alisifu uzuri na kasi wa meli ya New Butiama Hapa Kazi Tu inayozingatia usalama wa abiria na mizigo yao.

"Tumepata fursa ya Kwenda katika kisiwa cha Nansio, kule Ukerewe, kwa kutumia meli ya Kampuni hii ya MSCL ya New Butiama Hapa Kazi Tu, ni meli nzuri ambayo inatembea vizuri, tumefika mapema na tumekwenda na kurudi bila ya shida yoyote," alisema.

Aidha Mkurugenzi Rasilimali watu na...

inaendelea Uk. wa 5

Wakurugenzi Shirika la Meli la Zanzibar (SHIPCO) Mkurugenzi wa masoko Utafiti na Mipango Ndg. Jabir Sheha Amour (kulia) akiwa pamoja na Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala Bi. Saada Ali katika Meli ya New Butiama Hapa Kazi Tu.

Malenga Wetu

Bodi ya wakurugenzi MSCL wapigwa msasa na Uongozi Institute

Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) wamesifu utaratibu wa Serikali wa kutoa Mafunzo kwa Wajumbe wa Bodi za Mashirika ya Umma na Kampuni kwa nia ya kuwajulisha majukumu wanayotakiwa kuyatekeleza na kuyasimamia kwa maendeleo ya taasisi hizo za serikali.

Akizungumza baada ya Mafunzo hayo Mwenyekiti wa Bodi hiyo Mej. Jen. Mst, John Mbungo amesema kuwa wamefurahishwa na kitendo cha kupatiwa mafunzo kwa wajumbe wa Bodi pamoja na Menejimenti ya MSCL ili pande hizo ziweze kushirikiana katika kutekeleza majukumu ya Kampuni.

"Kwakweli yamefika katika kipindi muafaka kwasababu bodi ya MSCL ndio imeanza kutekeleza majukumu yake, mafunzo ni mazuri kuna mambo mengi ambayo watu hawayafahamu kwahivyo makampuni mengi ama mashirika yamekuwa yakiongozwa bila ya maarifa, bila ya ujuzi wowote ule, kwahiyo niwapongeze Uongozi Institute kwa kuandaa mada nzuri, mada mtambuka ambazo zinatujenga kiakili, kiuwezo ili tuweze kuwa viongozi bora zaidi ili tuweze kusimamia Kampuni hii kwa tija na mafanikio makubwa zaidi,"alieleza.

Mafunzo hayo yaliyotolewa baada ya mwezi mmoja tangu kuzinduliwa kwa Bodi hiyo yalijikita katika mada za Usimamizi wa rasilimali katika sekta za umma, kutambua majukumu ya kila mtendaji pamoja na uongozi na akili hisia (Emotional intelligence).

Kwa upande wake Katibu Mwelezi wa Chuo cha Uongozi Dkt. Fujo Hussein alisema kuwa mafunzo hayo ni muhimu kwa bodi mpya zinazoanza kutekeleza majukumu yake ili kuweza kuta ufanisi na tija katika kusimamia majukumu ya taasisi wanazozisimamia.

''Haya mafunzo ni ya lazima kwa Bodi zote ikiwa ni katika kutekeleza maagizo ya ofisi ya Rais katika kuhakikisha bod izote zinapata mafunzo haya''

Katika kelezea umuhimu wa mafunzo hayo kwa MSCL Mkurugenzi Mtendaji wa MSCL Eric Hamissi alisema kuwa mafunzo haya yataisaidia bodi kutambua majukumu yake pamoja na kutambua majukumu ya menejimenti ili kufanya kazi pamoja kuepusha muingiliano katika utendaji.

"Pia mafunzo haya yanatuwezesha tuweze kutimiza azma ya uanzishwaji wa hii taasisi, lakini Kubwa tuweze kiumsaidia Mheshimiwa Rais katika maono yake ya kuleta mapinduzi katika usafiri kwa njia ya maji kwa kutumia Kampuni yetu ya Huduma za Meli," alisema.

Mafunzo hayo yalifanyika makao makuu ya kampuni hiyo yaliopo jijini Mwanza yalioanza tarehe 13 Desemba 2022na kudumu kwa muda wa siku tatu yalifunguliwa na kiakao maaalumu kilichotoa muongozo wa namna mafunzo hayo yatakavyofanyika.

KAMPUNI YA MSCL

Na. Francis Kaswahili

Kampuni yetu ya umma, ya kuhudumia meli,
Inasimamia vyema, shughuli zote za meli,
Kwa dhati imesimama, yenyewe ndo muhimili,
M.S.C.L.ndiyo,inahudumiameli.

Kampuni hii hakika, tangu kuanzishwa kwake,
Malengo yamefikika, huduma bora ndo mwake,
Tena imeaminika, kwa nchi na watu wake,
M.S.C.L. ndiyo, inahudumia meli.

Nautaja pia mwaka, Kampuni ilipoanza,
Makao ikisimika, katika jijini Mwanza,
Kyela nako imefika, Kigoma ofisi mwenza,
M.S.C.L. ndiyo, inahudumia meli.

Elfu moja mia tisa, tisini na saba mwaka,
Kampuni ikawa hasa, hatamu yake kushika,
Kwa maziwa Victoria, Nyasa nalo Tanganyika,
M.S.C.L. ndiyo, inahudumia meli.

Ziwa Nyasa ni mchango, kwa uchumi wa taifa,
Malawi hasa ni lango, tumejizolea sifa,
Tuna meli za mizigo, kwa miliki ya taifa,
M.S.C.L. ndiyo, inahudumia meli.

Upande wa Tanganyika, Burundi Congo twafika,
Meli zetu zasifika, si haba twafaidika,
Biashara yafanyika, udugu kuimarika,
M.S.C.L. ndiyo, inahudumia meli.

Pia ziwa Victoria, upande wa Tanzania,
Nchi tatu twachangia, Kenya na Uganda pia,
Usawa wa mizania,Hamsini Tanzania,,
M.S.C.L. ndiyo,inahudumia meli.

Hapa ndio naishia, nilokusudi nilonga,
Vina havijanishia, kila jambo nikupanga
Usia nawaachia,nchi yetu kuijenga
M.S.C.L ndiyo, inahudumia meli,

SHUKRANI ZA KIPEKEE KWA KUFANIKISHA JARIDA HILI

BODI YA WAHARIRI

MWENYEKITI – ERIC B. HAMISSI
MHARIRI MKUU – ANSELM NAMALA
MHARIRI MSAIDIZI – ABDULRAHMAN SALIM

WAJUMBE

MHANDISI ABEL GWANAFYO
MHANDISI DEUSAN MSANGI
BARAKA BIGAMBO

BANDARI YA MWANZA KASKAZINI,
JENGO LA TPA, SAKAFU YA PILI
S. L. P. 2385, MWANZA,
Hotline: +255 739 606 600
Barua Pepe: info@mscl.co.tz
Tovuti: www.mscl.co.tz

HALIUZWI

JARIDA HILI IMEANDALIWA NA KUTOLEWA NA KAMPUNI YA HUDUMA ZA MELI